

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**  
**KUMWONDOA SPIKA AU NAIBU SPIKA KWENYE MADARAKA**

Taarifa  
ya  
Hoja ya  
Kumwondo-  
ndoa  
Spika au  
Naibu  
Spika

112. -(1) Mbunge yeyote anayetaka kutoa Taarifa ya hoja ya kumwondoa Spika au Naibu Spika kwenye madaraka chini ya Ibara Na. 84 na 85 za Katiba ya Nchi, atafanya hivyo kwa Maandishi na kumpelekea Katibu wa Bunge akitoa sababu kamili ya kuleta hoja hiyo.

(2) Katibu wa Bunge ataiweka hoja hiyo kwenye Orodha ya Shughuli za siku itakayoteuliwa, ambayo itakuwa mara baada ya siku kumi na nne kupita tangu taarifa hiyo ilipotolewa.

Masharti  
ya Hoja  
kupelekwa  
Bungeni

(3) Ili Hoja ya aina hiyo ikubaliwe kupelekwa Bungeni sharti itimize yafuatayo:-

- (a) iwe na tuhuma mahsusi;
- (b) iwe imetolewa maelezo kamili na sahihi, na yenye kueleweka;
- (c) isiwe na visingizio, matusi, kebehi, shutuma zenye lengo la kuharibu jina la mhusika.

Mtuhumiwa  
Kutokalia  
Kiti

(4) Spika au Naibu Spika, hatakalia Kiti cha Spika, wakati wa kujadili hoja ya kutaka kumwondoa madarakani, bali atakuwa na haki ya kujitetea wakati wa mjadala.

**(5) Spika au Naibu Spika, atakuwa ameondolewa kwenye Madaraka endapo zitapigwa kura zisizopungua theluthi mbili ya idadi ya Wabunge wote, za kuunga mkono hoja hiyo. Kura zitakuwa ni za siri.**

**(6) Spika au Naibu Spika anayetuhumiwa aweza kujiuzulu kuwa Spika au Naibu Spika kwa kutoa maelezo ya kujiuzulu kwake Bungeni kabla uamuzi juu ya hoja ya kumwondoa madarakani.**